



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA MKURANGA

Simu Na 0232402738,
Fax Na 023 2402706
Unapojibu tafadhali taja:



S.L.P 10
Mki
Pwani.

Kumb.Na. LD/MK/1628/27

17/4/2023

✓Mkurugenzi Mkuu,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC),
S.L.P.938
Dar es salaam

**YAH: UTAMBULISHO WA KAMPUNI YA KNAUF GYPSUM TANZANIA LIMITED
KUNUNUA VIWANJA NA.1,2,3 &8 KITALU 'G' KISEMVULE, WILAYA YA
MKURANGA**

Rejea mada tajwa hapo juu.

Ninawasilisha kwako nyaraka za manunuzi ya miliki ya viwanja Na.1,2,3 & 8 kitalu 'G' Kisemvule ambavyo awali vilimilikiwa na Kampuni ya **Lead Export and Mining Co. Ltd S.L.P.6569 Dar es salaam.**

Wamiliki wa kiwanja hiki kwa ridhaa yao wameuza viwanja hivi kwa Kampuni ya **Knauf Gypsum Tanzania Limited S.L.P.31873 Dar es salaam**, ambao sasa wamekamilisha taratibu zote za kisheria za kuhamisha miliki hii ikiwemo kulipa kodi stahiki ya mwaka wa fedha 2022/2023 na malipo ya ada za uhamisho kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya 1999 na Sheria ya Usajili wa hati Sura 334.

Kampuni ya **Knauf Gypsum Tanzania Limited** inamilikiwa na wageni (wasio raia) na hivyo uhamisho wa umiliki hizi kubeba sifa ya kuwa chini ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa mujibu Sheria Na.4 ya 1999 fungu la 19 &20, Tangazo la Serikali Na. 72 la tarehe 4/5/2001 pamoja na Sheria ya Uwekezaji Tanzania Na.26 ya 1997.

Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga inaitambulisha **Kampuni ya Knauf Gypsum Tanzania Limited** ili iweze kupewa Certificate of Incentives inayoonyesha uwekezaji kufanyika juu ya viwanja hivi au ikiwezekana certificate of Incentives waliyonayo kwenye uwekezaji uliosajiliwa iweze kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza viwanja hivi.

Nawasilisha kwako kwa hatua zaidi


Chagiye R.M
Kny:MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MKURANGA

Nakala: Mkurugenzi Mtendaji (W)
Mkuranga- Kwa taarifa

Knauf Gypsum Tanzania Limited
Dar es salaam-Kwa Ufuatiliaji